**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**
**MTIHANI WA KUHITIMU KIDATO CHA SITA**

**121/1** **KISWAHILI 1**

(Kwa watahiniwa Walioko na Wasiokuwa Shuleni)

**Muda: Saa 3** **Mwaka: 2024**

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina sehemu A na B zenye jumla ya maswali **nane (8)**.
2. Jibu maswali yote katika sehemu A na maswali **matatu (3)** kutoka sehemu B. Swali la **tano (5)** ni la lazima.
3. Sehemu A ina alama **arobaini (40)** na sehemu B ina alama **sitini (60)**.
4. Zingatia maagizo ya **kila sehemu** na ya **kila swali**.
5. Majibu yote yaandikwe kwa kalamu yenye wino wa **bluu** au **mweusi**.
6. Vifaa vya mawasiliano na vitu vyote visivyoruhusiwa **havitakiwi** katika chumba cha mtihani.
7. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

2 402121 200013

## SEHEMU A (Alama 40)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

1. Soma shairi lifuatalo kwa makini kisha jibu maswali yanayofuata:

Majira pia Nipashe, taarifa nazitoa
Na redio niwabishe, kama ikiwafikia
Majirani niwapashe, jambo nilokusudia
Ndege nimemfungua, wafugaji chukueni.

Ndege nawaelezea, tabia yake murua
Kucheka yake tabia, kununa hakuzoea
Wageni wakiingia, fadhila huwatendea
Ndege nimemfungua, wafugaji chukueni.

Tabia za firauni, hana ninawaapia
Na kuranda mitaani, si yake hiyo tabia
Marafiki wa kihuni, hapendi kuwasikia
Ndege nimemfungua, wafugaji chukueni.

Ni miaka ishirini, mimi nilimfungia
Hakuleta kisirani, kwa balozi kuamua
Wala kugoma jikoni, ugali kunipikia
Ndege nimemfungua, wafugaji chukueni.

Kisa niwaelezeni, tunduni nikamtoa
Msusa nambari wani, kisa si kisa alia
Hilo kosa namba wani, huzuni limenitia
Ndege nimemfungua, wafugaji chukueni.

Lingine lilochangia, tunduni nikamtoa
Kosa sugu nadhania, sijui kama sawia
Kufuga ndege Songea, Sijui kama sawia
Ndege nimemfungua, wafugaji chukueni.

Mara aliposikia, mwingine nimechukua
Tundu akalibomoa, porini akakimbia
Goti nikampigia, katu kanikatalia
Ndege nimemfungua, wafugaji chukueni.

**Maswali**

(a) Andika kichwa kinachofaa kwa shairi ulilosoma kwa maneno yasiyozidi matano.

(b) Mshairi anapotaja ndege katika shairi hili anamaanisha nini?

(c) Taja tabia tatu za ndege anayezungumziwa katika shairi.

(d) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika shairi ulilosoma.

(i) Murua

(ii) Firauni

(iii) Kisirani

(e) Sababu ipi ilimfanya mshairi amfungulie ndege wake aliyekuwa akimpenda?

(f) Katika ubeti wa mwisho mwandishi anaeleza ndege alichukizwa na nini?

(g) Funzo gani unalipata kutokana na shairi ulilolisoma?

2. Onesha miundo mitano ya kiima na mitano ya kiarifu kwa kutoa mfano kwa kila moja.

3. Bainisha vishazi katika sentensi zifuatazo, kisha taja aina ya kishazi ulichokibainisha:

(a) Mwanafunzi aliyefaulu vizuri amepata ufadhili.

(b) Sikukuu ya sabasaba inakaribia mimi nitakwenda uwanjani.

(c) Mwanao akililia wembe usimpe.

(d) Ungemuona simba ungejificha mapema.

(e) Kisima ambacho kimejaa tope tupu wananchi hawakipendi.

4. Mtumiaji wa lugha ya Kiswahili anapaswa kuzingatia misingi gani? Fafanua kwa ufupi misingi mitano kwa kutumia mfano kwa kila moja.

**SEHEMU B (Alama 60)**

Jibu maswali **matatu (3)** kutoka sehemu hii. Swali la **tano (5)** ni la lazima.

5. Fafanua sifa sita za tafsiri ya matini za kisayansi na kiteknolojia kwa kutoa mfano kwa kila moja.

6. Andika insha ya maneno yasiyozidi **mia nne** na yasiyopungua **mia tatu na hamsini** kuhusu sababu na athari za ndoa za utotoni.

7. Vyombo vya habari vilikuwa na mchango gani katika kukuza Kiswahili nchini Tanganyika wakati wa ukoloni ? Fafanua kwa kutumia hoja tano.

8. Kamati ya lugha ya Kiswahili ya Afrika Mashariki iliyoanzishwa mwaka 1930 kwa lengo la kukuza na kueneza lugha ya Kiswahili ilikuwa na majukumu mbalimbali. Eleza majukumu sita yaliyotekelezwa na Kamati hiyo.